International Journal of Social and Development Concerns

ISSN 2524-1478 (Online)

Vol. 29| Post COVID-19 Recovery and Sustainable development
Vol. 29 Article 8 | October 3, 2025
Copyright © 2025 The International Journal of Social and Development Concerns (IJSDC) All Rights Reserved
(An International Publisher for Academic and Scientific Resources)

# Usimilishaji wa Vipengee vya Maandishi ya Kale: Mfano wa Tenzi za Fumo Liyongo na Mwana Kupona

**Waandishi:** [1]Evangeline Makena Mitambo, [2]Dorcas M. Musyimi na [3]Allan Mugambi
[1,2&3]Chuo Kikuu Cha Chuka. **Tovuti :** ***www.chuka.ac.ke***
**Mawasiliano:** Mitambo Evangeline Makena. **Barua Pepe:** evamitambo@gmail.com
***Cite as:*** *Mitambo, E. M., Musyimi, D. S., & Mugambi, A. (2025). usimilishaji wa Vipengee vya Maandishi ya Kale: Mfano wa Tenzi za Fumo Liyongo na Mwana Kupona. International journal of social and development concerns, 29(8), 98–113. https://doi.org/10.5281/zenodo.17288222*

**Chief Editor** Web: www.ijsdc.org Email: info@ijsdc.org

**Editing Oversight** Impericals Consultants International Limited

***Abstract:*** *Tenzi za kale za Kiswahili kama Fumo Liyongo na Mwana Kupona ni hazina kubwa ya urithi wa kifasihi, historia na utamaduni wa Waswahili. Hata hivyo, tenzi hizi ziliundwa kwa hadhira ya watu wazima na zimejaa lugha ya kale, mafumbo, mitindo ya kishairi tata pamoja na maudhui mazito ya kifalsafa na kidini ambayo watoto hawawezi kuyafikia kwa urahisi. Hali hii inaleta changamoto ya jinsi urithi huu muhimu unaweza kuwasilishwa kwa watoto bila kupoteza maana yake ya asili. Kwa hiyo, utafiti huu unalenga kuchunguza namna ambavyo vipengele vya msingi vya tenzi za kale vimebadilishwa kupitia usimilisho ili kulenga hadhira ya watoto bila kupoteza utambulisho wa kihistoria na kitamaduni wa Waswahili. Wasanii wa kisasa wamefanya jitihada za kusimilisha tenzi hizo kwa kuzibsahilisha kuwa fasihi ya watoto. Hata hivyo, tafiti za kina kuhusu jinsi masimilisho haya yamesahilishwa na athari zake katika uwasilishaji wa historia, utamaduni na maadili kwa watoto bado ni chache. Makala hii inachunguza ukarabati wa vipengee katika tenzi za kale ili kulenga hadhira ya watoto, kwa kuzingatia mifano ya Utenzi wa Fumo Liyongo (UwFL) na Utenzi wa Mwana Kupona (UwMK). Data ya utafiti ilikusanywa kupitia usomaji wa makini wa matini chasili mathalan; UwFL na UwMK pamoja na matini lengwa; Kisa cha Fumo Liyongo (KcFL), Wasifu wa Mwana Kupona (WwMK) na Mkasa wa Shujaa Liyongo (MwSHL). Uchambuzi ulifanywa kwa misingi ya Nadharia ya Usimilisho ya Hutcheon (2013). Ukarabati uliobainika kutokana na utafiti huu ni pamoja na: urahisishaji wa lugha ya Kiswahili cha kale kwa kutumia Kiswahili sanifu na sentensi fupi; kupunguzwa kwa maudhui magumu ya kidini na kuelekezwa katika mafunzo ya maadili; kuongeza wahusika na kuwapa tabia zinazolingana na ulimwengu wa watoto; kubadilisha muundo wa kishairi kuwa nathari na mashairi mepesi; kugawanya simulizi katika sura fupi na kuongeza michoro inayosaidia uelewa wa watoto. Vilevile, mandhari na miji ya kihistoria kama Lamu na Pate iliwasilishwa kwa namna inayodumisha utambulisho wa Kiswahili. Kutokana na hitimisho kwamba usimilisho umesababisha urahisishaji wa lugha na kupunguzwa kwa maudhui mazito ya kifalsafa, hali iliyoacha watoto na ufahamu mdogo wa utajiri wa ushairi wa kale, utafiti unapendekeza kuwa mashirika ya kijamii na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yashirikiane na shule ili kuunda vipindi vya kusoma ambapo tenzi asilia na kazi zilizosimilishwa zitaweza kufundishwa kwa pamoja ili kuimarisha ujifunzaji wa watoto.*

***Maneno makuu**: Fasihi ya Watoto, Hadhira ya Watoto, Matini,Ttenzi za Kale, Usimilisho, Vipengee*

## 1.1 Utangulizi

Fasihi ni sanaa inayolenga kushughulikia maisha yanayohusu jamii kwa jumla kama anavyosema Nkwera (1979). Nkwera (mtaje) anaendelea kuhoji kuwa, fasihi ni mojawapo ya utamadumi wa jamii kwa kuwa hueleza hali ya maisha katika jamii kwa jumla. Fasihi ya watoto ni taaluma inayojisimamia

ingawa mizizi yake ipo katika fasihi kwa jumla.

Fasihi ya watoto kulingana na Wamitila (2008) ni sanaa ambayo kimsingi hurejkelea matini au kazi ambazo hadhira yake kubwa ni watoto. Wamitila (mtaje) anaedelea kusema kuwa, fasihi ya watoto ni kazi inayowarejelea watoto kwa kuangazia dhamira na maudhui. Fasihi hii imeanza kuchunguzwa kwa upekee katika karne ya kumi na nane. Wamitila (mtaje) anasema kuwa, fasihi iliyotungiwa hadhira ya watoto inapolinganishwa na ile iliyotungiwa hadhira ya watu wazima ni mpya sana. Hii ni kwa sababu, hutumia lugha nyepesi ili kueleweka kwa urahisi na hadhira ya watoto.

Kulingana na Sanders (2006), usimilisho wa vitabu kwa usomaji wa watoto katika mashirika makubwa na madogo ya uchapishaji kunaonyesha dhamira ya kupanua mipaka ya usomaji katika madarasa na maktaba. Waandishi hulazimika kufanyia mabadiliko kazi zilizotungiwa hadhira ya watu wazima ambazo zimevuka mipaka na kuingia katika fasihi ya watoto mabadiliko ili kufaa hadhira ya watoto. Kuna vitabu ambavyo vimesimilishwa kwa ajili ya watoto jambo ambalo huwafanya watoto wawe washiriki halali wa utanzu uliosimilishwa. Ubadilishaji wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto hutoa fursa ya kusambaza maadili ya kitamaduni, mila na simulizi za kihistoria kwa watoto kwa njia inayovutia na inayoeleweka. Hivyo, makala haya yamelenga kuhakiki usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto kwa kuchunguza jinsi tenzi za kale zilizosimilishwa kuwa fasihi ya watoto zinaweza kutumiwa kama njia ya kukuza uelewa wa kihistoria na kitamaduni kwa watoto.

### 1.2 Suala la Utafiti

Tenzi za kale za Kiswahili kama *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Utenzi wa Mwana Kupona* ni hazina kubwa ya urithi wa kifasihi, historia na utamaduni wa Waswahili. Hata hivyo, tenzi hizi ziliundwa kwa hadhira ya watu wazima na zimejaa lugha ya kale, mafumbo, mitindo ya kishairi tata pamoja na maudhui mazito ya kifalsafa na kidini ambayo watoto hawawezi kuyafikia kwa urahisi. Hali hii inaleta changamoto ya jinsi urithi huu muhimu unaweza kuwasilishwa kwa watoto bila kupoteza maana yake ya asili. Kwa hiyo, utafiti huu unalenga kuchunguza namna ambavyo vipengele vya msingi vya tenzi za kale vimebadilishwa kupitia usimilisho ili kulenga hadhira ya watoto bila kupoteza utambulisho wa kihistoria na kitamaduni wa Waswahili.

### 1.3 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti umeongozwa na nadharia ya Usimilisho kwa mtazamo wa Linda Hutcheon (2013). Mhimili unaosisitiza kwamba msingi wa usimilisho ni hadithi ulisaidia katika uchanganuzi kwa sababu tenzi za kale kama Fumo Liyongo na Mwana Kupona zilikuwa na hadithi ndefu, zenye maumbo ya kishujaa, kihistoria na kifalsafa ambazo hazingeweza kufaa moja kwa moja kwa watoto. Kwa kutumia kipengee hiki cha nadharia, utafiti ulionyesha namna waandishi wa masimulizi mapya (*Kisa cha Fumo Liyongo, Mkasa wa Shujaa Liyongo* na *Wasifu wa Mwana Kupona*) walivyoshikilia hadithi kuu bali wakaikarabati, kuirahisisha na kuielekeza ili iweze kufahamika kwa watoto bila kupoteza kiini chake. Mhimili wa pili unaoshikilia kuwa usimilisho si nakala ya moja kwa moja bali ni mchakato wa kusahirisha hadithi kulingana na hadhira na mazingira mapya ulisaidia namna hadithi ya maandishi ya kale imesahirishwa. Katika muktadha huu kusahirisha hadithi ni kuondoa vipengee vizito kama lugha tata ya Kiswahili cha kale au mafundisho mazito ya kifalsafa na kuviweka kwa namna inayomfaa mtoto kisaikolojia. Mtazamo wa Hutcheon wa usimilisho kama ukarabati wa kina wa kazi Fulani ulisaidia kueleza jinsi tenzi za kale, ambazo zilitumia bahari ya mashairi yenye tarakimu na vina, zilivyogeuzwa kuwa masimulizi ya nathari yenye lugha nyepesi na picha za kuvutia. Pia ilionyesha ukarabati wa

muundo mzima wa tenzi kutoka katika mashairi yenye mpangilio wa kitarakimu hadi riwaya na masimulizi ya hadithi kwa watoto. Usimilisho kama utafsiri upya na umbaji upya ni mhimili uliotumika kuonyesha kwamba wasanii wa usimilisho hawakubadili tu lugha au muundo, bali waliunda upya kazi kwa kuipa maana mpya inayomfaa mtoto.

### 1.4 Mapitio Ya Maandishi

Usimilisho ni aina ya tafsiri ambayo hujitokeza katika matini hivi kwamba matini hiyo hubadilika kiasi cha kuwa yanatambuliwa kama kiwakilishi cha matini chasili kama anavyoeleza Baker (2001) katika masomo ya tafsiri. Usimilisho ni tofauti na tafsiri kwa kuwa, tafsiri ni hali ya kushurutisha inayotekelezwa katika matini chasili. Wakati wa usimilisho, matini chasili hubadilishwa. Mawazo ya Baker (mtaje) yalimwongoza mtafiti katika kujadili namna usimilisho ulisahilisha mawazo ya kale na kuyawasilisha kupitia mawazo ya kisasa yanayolingana na mtoto wa kisasa katika fasihi ya watoto kwa lengo la kukuza fasihi ya watoto.

Lhermitte (2005) anadai kuwa wakati wa mwanzo usimilisho ulitumika kurejelea aina mojawapo ya tafsiri kabla ya maelezo kuhusu ugeuzaji ambao hufanyiwa kazi za fasihi kuwa kazi za aina tofauti na ile ya mwanzo. Kulingana na Lhermitte (mtaje), usimilisho ni dhana inayohusiana na tafsiri unapozingatia lengo au dhima. Dhana hizi mbili kulingana na lengo zinahusu kuhamisha ujumbe kutoka matini moja hadi matini nyingine kwa kudumisha ualisia wa matini ya kwanza. Katika muktadha huu, usimilisho na tafsiri ni dhana ambazo dhima yazo kuu ni mawasiliano. Utafiti huu ulinufaika na maelezo ya Lhermitte (mtaje) katika kutathmini vipengee vya tenzi teule vilivyosimilishwa.

Punzi (2007) katika utafiti wake kuhusu usambazaji wa fasihi kupitia vyombo vya habari, anahoji kuwa, hali ambapo ujumbe huvuka mipaka ambayo inatenganisha njia tofauti za mawasiliano huchukuliwa kuwa mwingiliano matini wa njia za mawasiliano. Kuna uwezekano wa kazi ya fasihi kufasiliwa kutoka njia fulani ya mawasiliano hadi njia nyingine tofauti hadi pale ambapo huibuka kuwa na sura tofauti ambazo zinaibainisha. Kama anavyosema Punzi (mtaje), uvukaji wa mipaka ya njia za mawasiliano hali ambayo ni sawia na ile ya mipaka ya tanzu, ni hali ambayo imekuwa kwa muda mrefu katika fasihi. Kugeuza matini ya fasihi na kuiweka katika umbo tofauti na lile la awali huku ukizingatia njia tofauti ya mawasiliano ni mwingiliano wa njia za mawasiliano. Mchakato ambao unahusishwa na hali hizo hujulikana kama usimilisho. Mawazo ya Punzi (mtaje) yalimfaa mtafiti katika kujadili vipengee vya tenzi teule za kale vilivyosimilishwa kuwa fasihi ya watoto katika vitabu teule kama njia tofauti ya kurahisisha mawasiliano.

Utafiti wa Dean (2009) kuhusu usimilisho wa historia na fasihi kama sinema ulibaini kuwa, tafsiri kupitia njia tofauti za mawasiliano huwa ni usimilisho. Dean (mtaje) anaendelea kusema kuwa, usimilisho hubainika kutokana na matumizi ya malighafi muhimu, mbinu tofauti na kanuni za kiubunifu. Hivyo, usimilisho unaweza kuchukuliwa kuwa hali ya kuhamisha ujumbe kutoka njia moja ya mawasiliano na kuuwasilisha kwa kutumia njia tofauti na ile ya awali. Kulingana na Dean (mtaje), usimilisho ni mwingiliano matini ambao huwa na dhima ya kuunda kazi za jadi mpya. Utafiti wa Dean (mtaje) unalingana na utafiti huu kwa kuwa tafiti zote zinahusu usimilisho ila kuna tofauti kwa kuwa utafiti wa Dean (mtaje) ulihusu usimilisho wa historia na fasihi tofauti na utafiti huu unaohusu usimilisho wa tenzi za kale. Hata hivyo, utafiti wa Dean (mtaje) ulimwongoza mtafiti katika kujadili vipengee vya tenzi za kale teule vilivyosimilishwa.

Anavyosema Balodis (2012) kutokana na utafiti wake kuhusu usimilisho wa ukweli na hadithi kama maigizo ni kuwa, kumekuwa na mbinu kadha ambazo wanaotunga kazi za fasihi wamekuwa wakitumia kama njia ya kuibuka na mahusiano ya tanzu mbalimbali za fasihi. Usimilisho ni mojawapo ya njia ambayo watunzi wamekuwa wakitumia. Hii ni ile hali ambapo matini fulani ambayo inapatikana katika utanzu fulani wa fasihi inapewa sifa za matini nyingine tofauti ambayo inapatikana katika utanzu mwingine tofauti wa fasihi na matini hiyo. Kulingana na historia ya fasihi ya Kiswahili, tenzi maarufu zilisimilishwa kuwa masimulizi ya kuhadithiwa. Wagiriki walibuni masimisho ya tamthilia ambazo zilitokana na hadithi za visasili, historia yao na tendi. Shakespear ambaye ameandika tamthilia mbalimbali, alijitoma katika uwanja wa usimilisho na kusimilisha hadithi zilizohusu mapenzi, tamthilia za waandishi mbalimbali na historia. Wasanii huweza kuibuka na kazi tofauti na ile ya awali baada ya usimilisho kutokana na ubunifu na tajriba yao. Utafiti wa Balodis (mtaje) ni sawa na utafiti huu kwa kuwa tafiti zote zinahusu usimilisho; tofauti ni kuwa, utafiti wa Balodis (mtaje) ulihusu usimilisho uliolenga uwanja wa maigizo ila utafiti huu unalenga uwanja wa fasihi andishi ya watoto. Maelezo ya Balodis (mtaje) yalimwogoza mtafiti kuchunguza vipengee vya tenzi za kale teule vilivyosimilishwa.

Katika maelezo yake Senkoro (2011) kuhusu mtindo ni kuwa, ni ile hali ya upekee wa kuunda kazi ya fasihi ambao hutofautisha msanii mmoja kutoka kwa mwingine kutokana na hisia alizo nazo msanii. Fasihi ya watoto hutumia mtindo wa michoro au picha. Ngugi (2011) anashadidia haya kwa kusema kuwa, kazi za watoto zinastahili kuwa na michoro au picha. Kulingana na Ngugi (mtaje), michoro humfanya mtoto avutiwe na kazi anayoisoma na kuwa makini kwa kazi ile hivi kwamba huona uhalisia wa kile anachokisoma. Maelezo haya yatamfaa mtafiti katika kujadili vipengeee vya tenzi za kale teule vilivyosimilishwa.

Samwel (2015) anasema kuwa, fasihi ya watoto inastahili kuwa na dhamira zisizo changamani. Kulingana na Samwel (mtaje), dhamira ni lengo, kusudio au wazo muhimu ambalo linaangaziwa katika kazi ya fasihi. Mara nyingi, kazi za watoto huwa na dhamira sahili (Samwel, mtaje). Hii husaidia katika kurahisisha ujumbe unaokusudiwa ili ueleweke na mtoto kulingana na anachokusudia mwandishi. Katika kazi ya watoto ambayo hutumia dhamira changamani, mtoto hufurahia tu picha bila kuelewa kilichoelezwa na mwandishi wa kazi hiyo. Ngugi (mtaje) anashadidia haya anaposema kuwa, vitavu ambavyo vinaandikwa na kuteuliwa kwa ajili ya kusomwa na watoto, vinahitaji kulingana na umri na uwezo wa wa watoto ili kujenga mielekeo chanya kuhusu vitabu vya watoto. Mwandishi anastahili kuelewa watoto katika viwango mbalimbali vya umri ili kuzingatia kiwango cha uelewa cha kila mtoto wakati wa kutunga kazi za fasihi. Hii ni kwa kuwa, mada ngumu na tata humchocha msomaji ambaye hajamakinika katika harakati za usomaji. Katika uwasilishaji wa kazi za watoto, ni muhimu kuzingatia usahili kwa kuwa watoto wanastahili vitabu vinavyoshughulikia mada mbalimbali na ambavyo vimesimilishwa kwa kuzingatia talanta za watoto. Maarifa haya yalimwongoza mtafiti katika kujadili vipengee vinavyomchochea mtoto kupata uelewa wa kihistoria na kitamaduni kwa watoto.

Utafiti wa Kairu (2005) kuhusu uhalisia wa mtindo wa Ken Walibora katika vitabu vya *Ndoto ya Amerika* (2001), *Mgomba Changaraweni* (2003) na *Mtu wa Mvua* (2003) ulibaini kuwa, msimilishi anaweza kuisimilisha kazi ya fasihi akiwa na lengo la kuifanya kazi husika iangazie hadhira anayokusudia kwani kazi ya fasihi iliyolenga hadhira ya watu wazima ilisimilishwa ili isomwe na hadhira ya watoto. Hadhira ya watoto imekuwa ikisimilishiwa vitabu vya fasihi vilivyoandikwa kwa ajili ya hadhira ya watu wazima ili waweze kuvisoma. Hadithi zimesimilishwa ili kuweza kufasiriwa kwa wepesi na hadhira ya watoto. Baada ya wakoloni Wazungu kuingia, walileta hati za Kirumi za kuandika

na hivyo kufanikisha usimilisho. Utafiti wa Kairu (mtaje) unakaribiana na utafiti huu kwa kuwa tafiti zote zinahusu fasihi ya watoto. Hata hivyo, kuna tofauti kwa kuwa utafiti huu unahusu uwasilishaji wa historia na utamaduni kwa hadhira ya watoto kupitia usimilisho ila utafiti wa Kairu (mtaje) ulihusu mtindo aliotumia Ken Walibora kutunga fasihi ya watoto. Kwa kuwa tenzi za kale teule zilisimilishwa ili kulenga hadhira ya watoto, maelezo ya Kairu (mtaje) yalimfaa mtafiti katika kutathmini vitabu teule ambavyo ni masimilisho ya tenzi za kale teule kwa lengo la kuchunguza vipengee vya tenzi za kale teule vilivyosahilishwa.

Naye Kaui (2015) ni kuwa, usimilisho ni fani ambayo uhusu uendelezaji ambao unahusu mwingiliano matini huku utanzu ukiwa kiini cha utanzu wa riwaya na ule wa hadithi fupi. Haya yalitoka na tathmini ya usimilishwaji riwaya ya *Siku Njema* na *Utengano* na hadithi fupi ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Kenya. Kaui (mtaje) alizingatia misingi ya Nadharia ya Usimilisho kwa maoni ya George Bluestone pamoja na Nadharia ya Uigizaji kwa maoni ya Aristotle. Tanzu za Riwaya na hadithi fupi alizochunguza Kaui (mtaje) zilionyesha sifa za kitamthilia na hivyo kubaini kuwa mbinu zinazohusiana na usimilisho ni za kimwingiliano matini. Kaui (mtaje) alibaini kuwa, ili masimilisho yaweze kuwa aminifu kwa matini chasili, inategemea jinsi msimilishaji atatumia ustadi wakati wa kutumia mbinu za mwingiliano wa matini. Tofauti na utafiti huu ambao ulihakiki usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto, utafiti wa Kaui (mtaje) ulitathmini usimilisho katika fasihi andishi kama sanaa ya maonyesho. Hata hivyo, utafiti wa Kaui (mtaje) umemsaidia mtafiti kupanua mawazo kuhusu usimilisho. Mtafiti amepata mwanga wa kujadili vipengee vinavyohitaji kusimilishwa ili kuwalenga watoto.

Kulingana na Omuya (2017) alipokuwa akichunguza usimilisho wa *Biblia* kama fasihi ya watoto, usimilisho umekuwa tangu enzi zilizokuwa za wakoloni. Usimilisho ulianza pindi tu wakoloni waliposimilisha kazi zilizoandikiwa hadhira ya watu wazima kuwa kazi ambazo zinalenga hadhira ya wtoto. Katika utafiti wake, Omuya (mtaje) alifanya ulinganisho wa matini chasili na matini lengwa huku akilenga kuchunguza iwapo kuna mabadiliko mbayo yalifanyiwa matini chanzi wakati wa kuisimilisha matini hiyo. Omuya (mtaje) alijihusisha na usimilishwaji wa *Biblia* kama kitabu kitakatifu ambacho waandishi walikiandika huku wakiongozwa na tamaduni na maarifa maalum ya thiolojia tofauti na utafiti huu ambao umeshughulikia vitabu vilivyoandikwa na waandishi ambao walihitaji ujuzi wa kisanaa bila kutegemea thiolojia. Hata hivyo, kazi ya Omuya (mtaje) imemfaa mtafiti hasa katika kutathmini usahilishaji uliofanyiwa tenzi za kale teule.

Mwendwa (2020) alitafitia usimilishwaji wa vielelezo katika hadithi ya *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (2015) na *Wasifu wa Mwana Kupona (*2008) na machango wake katika kuendeleza ujumbe kwa kuzingatia Nadharia ya Usimilisho. Mwenda (mtaje) alitambua kwamba, katika hadithi za watoto, vielelezo huenda vikatumika kama mbinu ya kupasha ujumbe ulioandikwa kwenye matini. Matumizi ya vielelezo huenda yakarahisiha na hata kupanua uelewa wa matini hivyo lengo la mwandishi na mchoraji kuafikiwa. Iwapo vielelezo vitatumika vibaya, huenda kukawa na kutoeleweka kwa ujumbe alionuia mwandishi wa matini. Mtafiti amejadili usimilisho wa tenzi za kale ili kuchunguza jinsi waandishi wametumia mandhari kuendeleza ploti katika fasihi ya watoto tofauti na Mwenda (mtaje) aliyechunguza usimilisho wa vielelezo ili kupitisha ujumbe kwa watoto. Mintarafu ya hayo, mtafiti amenufaika na utafiti wa Mwendwa (mtaje) katika kujadili vipengle muhimu katika tenzi za kale teulevilivyosimilishwa.

Kupitia marejeleo ya tafiti tangulizi, ni bayana kuwa, tafiti za awali zinatoa mwelekeo kwa mtafiti kuhusiana na usimilisho. Ingawa kuna tafiti zimefanywa kuhusu usimilisho katika fasihi, watafiti wa awali hawajashughulikia usimilisho wenye nia ya kujadili usahilishaji wa vipengee vya tenzi za kale ili kulenga hadhira ya watoto. Kwa sababu hii, utafiti huu ulihakiki usimilisho wenye dhamira ya kuigeuza fasihi andishi ya watu wazima kwa namna ambavyo mwandishi alidhamiria ili kutumika kama fasihi ya watoto. Utafiti huu umehakiki usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto kwa kutathmini ukarabati uliofanyiwa tenzi tenzi za kale teule ili kuibuka na vitabu vinavyoeleweka na hadhira ya watoto.

## 1.5 Njia Za Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika muundo wa kimaelezo kwa kuwa ulihusisha kueleza na kufafanua mchakato wa usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto. Njia hii ilirahisisha kuelewa kwa undani ukarabati uliofanyiwa vipengee vya tenzi za kale zilizoteuliwa. Ili kupata data sahihi, utafiti ulitumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui ambapo vitabu teule vya *Kisa cha Fumo Liyongo*, *Mkasa wa Shujaa Liyongo* na *Wasifu wa Mwana Kupona* vilisomwa kwa makini na kulinganishwa na tenzi asilia mathalani: *Fumo Liyongo* na *Mwana Kupona*. Kupitia uchambuzi huu, usahilishaji wa lugha, wahusika, maudhui na mbinu za kifasihi yaliweza kubainishwa. Vilevile, utafiti huu ulitumia mbinu ya linganishi ili kulinganisha baina ya utenzi wa *Fumo Liyongo* na usimulizi wake katika *Kisa cha Fumo Liyongo* na *Mkasa wa Shujaa Liyongo* pamoja na utenzi wa *Mwana Kupona* na usimulizi wake katika *Wasifu wa Mwana Kupona*. Njia hii ilirahisisha kubaini tofauti na usahilishaji uliosababishwa na usimilisho. Sambamba na hili, uchambuzi wa nadharia ulitumiwa ambapo mihimili ya nadharia ya usimilisho ilitumika kueleza na kuhalalisha ukarabati uliofanyika ili kazi teule ziweze kuwafaa watoto. Kuhusu sampuli, utafiti huu ulitumia uteuzi makusudi (purposive sampling) ambapo vitabu vitatu pekee vilichaguliwa kwa kuwa vinahusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti na vimeandikwa mahsusi kwa ajili ya hadhira ya watoto.

## 1.6 Ukarabati Wa Vipengee Teulevya Tenzi Za Kale Ili Kulenga Hadhira Ya Watoto

Uchambuzi unaonyesha kuwa usimilisho umefanyika kwa kusahilisha vipengee kama lugha, mtindo wa usimulizi, maudhui, uwasilishaji wa wahusika na urefu wa kazi, ili kufanya hadithi ziwe rahisi kueleweka na kufundisha maadili kwa watoto. Hivyo, usimilisho unatambulika kama njia ya kufanikisha uwasilishaji wa historia, utamaduni, na maadili ya Kiswahili kwa kizazi kipya. Nadharia ya Usimilisho ya Hutcheon (2013), usimilisho ni tendo la ubunifu linalohusisha ubadilishaji wa kazi asilia kwa kuzingatia muktadha mpya. Vipengele vilivyobadilishwa ni kama vifuatavyo:

### *Kipengee cha Lugha*

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), tenzi hutumia lugha ya kipekee ikilinganishwa na lugha inayotumika katika tanzu nyingine za fasihi. Lugha ni chombo muhimu katika utunzi na uwasilishaji wa kazi za kifasihi. Katika usimilisho wa tenzi teule za kale, katika fasihi ya watoto, lugha imebadilishwa kwa njia mbalimbali ili kufanikisha mawasiliano na hadhira ya watoto. Nadharia ya Usimilisho ya Linda Hutcheon (2013) inabainisha kuwa, kazi ya kifasihi inaposimilishwa katika muktadha mpya, lazima ibadilishwe kwa njia ya kisanii ili kuendana na hadhira na mazingira mapya. Hivyo, mabadiliko ya lugha yanayoonekana katika kazi teule si ya kiholela bali ni ya kimakusudi na yenye msingi wa kimaudhui. Usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto unahusu ukarabati wa vipengee mbalimbali mojawapo ikiwa lugha. Wakati wa kutunga masimilisho teule, waandishi wa mebadilisha kipengele cha lugha kama ifuatavyo:

### *Urahisishaji wa Maneno*

Katika muktadha wa Nadharia ya Usimilisho ya Hutcheon (taje), kipengee hiki cha lugha kinaonyesha wazi mchakato wa uundaji upya wa kazi asilia ili kuendana na hadhira mpya ya watoto. Hutcheon anasisitiza kuwa usimilisho si tafsiri ya moja kwa moja, bali ni tendo la kisanii la kukarabati maumbo, mitindo na lugha ili kuibua maana mpya inayofaa mazingira mapya ya mapokezi. Kwa mujibu wa dhana hii, urahisishaji wa lugha katika *KcFL*, *WwMK* na *MwSHL* ni mfano dhahiri wa usimilisho wa kimakusudi. Wamitila (mtaje) anaeleza kuwa, tenzi za kale zilitumia lugha ya kishairi, ya kale na yenye maneno ya Kiarabu au ya kilahaja ambayo ni magumu kwa watoto. Hivyo, katika mchakato wa usimilisho, waandishi wameunda upya lugha hii ili iweze kueleweka na kuvutia hadhira changa.

Kwa mfano, katika *UwMK*, maneno kama **"***mteshiteshi***"** na **"***faradhi***"** yaliyokuwa na mizizi ya kidini na kihistoria yamekarabatiwa katika *WwMK* kuwa lugha rahisi kama **"**kuwa mcheshi**"** na **"**kuwa na nidhamu**"**. Hatua hii inaonyesha kile ambacho Bluestone (1957) anakiita *"*kubadilisha maumbo ili kudumisha maana katika muktadha mpya*."* Hapa, usimilisho unalenga kuhifadhi dhamira ya maadili na dini ila kwa kutumia lugha inayomfikia mtoto moja kwa moja bila ugumu wa kisemantiki.

Vivyo hivyo, katika *KcFL*, usemi wa kishairi **"***kimo kawa mtukufu***"** kutoka *UwFL* umekarabatiwa kuwa **"***Liyongo kakua mwilini***,** *hashindiki michezoni***"**, ambao ni wa moja kwa moja na unaendana na uelewa wa mtoto. Hili linadhihirisha ushirikiano wa kimakusudi kati ya chanzo na matini lengwa kwa mujibu wa Nadharia ya Usimilisho, ambapo usimilisho hufanyika bila kupoteza kiini cha kazi asilia. Aidha, usimilisho huu unalenga zaidi ufahamu na burudani ya watoto. Kwa mujibu wa Ngugi na Nabea (2011), vitabu vya watoto vinapaswa kutumia lugha sahili na ya moja kwa moja ili kurahisisha uelewa. Hii inaendana na hoja ya Goodman (1976) kwamba, kazi inapohamishwa katika muktadha mpya, muundo wa usemi lazima ubadilishwe ili kuafiki hadhira lengwa. Kwa hiyo, ukarabati wa lugha ya tenzi za kale ni hatua ya kimakusudi inayofafanua falsafa ya usimilisho kama mchakato wa kubadili na kuumba upya badala ya kuiga au kutafsiri.

### *Urahisishaji wa Miundo ya Kisarufi*

Muundo ni msuko, mwingiliano na uwiano wa vipengele vyote vinavyojenga kazi nyingine ya sanaa (Njogu na Chimerah, 1999). Usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto si kurahisisha maandishi tu bali ni jitihada yenye kusudi iliyobuniwa kuunganisha wasomaji wachanga na utajiri wa urithi wao wa kitamaduni. Kwa mujibu wa nadharia ya Usimilisho, Hutcheon (mtaje) anaeleza kuwa, lugha ni mojawapo ya vipengee vinavyoweza kubadilishwa wakati wa usimilisho ili kazi lengwa iendane na hadhira lengwa.

Katika usimilisho wa tenzi za kale teule, sentensi zimebadilishwa kuwa fupi, sahili na zenye mtiririko wa moja kwwa moja. Mabadiliko ya miundo ya kisarufi si jambo la hiari tu bali ni kitendo cha kimakusudi cha kifasihi cha kufanya matini chanziitumike katika muktadha mpya baada ya ukarabati. Kulingana na Starrs (2006) mhitifaki wa Nadharia ya Usimilisho, kila usimilisho ni kitendo cha kufasiri upya na kubadilisha kazi chasili ili iendane na hadhira mpya, huku ikihifadhi upekee fulani wa matini chasili. Katika kusimilisha vipengee vya tenzi wa kale teule, miundo tata ya kishairi na sentensi ndefu zilikarabatiwa kuwa maandishi ya moja kwa moja na rahisi. Ukarabati wa miundo ya kisarufi si jambo la hiari tu bali ni kitendo cha kimakusudi cha kifasihi cha kufanya matini chanzi itumike katika muktadha mpya baada ya ukarabati. Hutcheon (mtaje) anaeleza kwamba, kila usimilisho ni kitendo cha kufasiri upya na kuunda upya kazi chanzi ili iendane na hadhira mpya, huku ikihifadhi upekee fulani wa matini chanzi. Kwa hivyo, kukarabati miundo tata ya kishairi kuwa sentensi fupi na wazi ni hatua ya kuiweka

kazi katika muktadha mpya unaomfaa mtoto. Ni wazi kwamba, tenzi za kale zilizotumia miundo tata ya kishairi na sentensi ndefu zilisahilishwa kuwa maandishi ya moja kwa moja na rahisi kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao.

*Pete sikose zandani,*
*Hina sikose nyaani,*
*Wanda sitoe matoni,*
*Na nshini kuitia*
*(UwMK ubeti 41)*

*Masikioni huvae herini, utie na wanja machoni pamoja na hina kwenye viganja vya mikono na miguu.*
*(WwMK uk. 12)*

Hapa, muundo wa kishairi wenye vina na mizani umevunjwa na kukarabatiwa kuwa taarifa rahisi ya kimaelezo. Ukarabati huu unathibitisha hoja ya Bluestone (mtaje) kwamba, usimulizi unapotoka katika mfumo wa kishairi kwenda kwenye nathari, mfumo wa uwasilishaji wa maana hubadilishwa kulingana na hadhira mpya.

Vivyo hivyo, *UwFL* ulitumia lugha ya kishairi, lakini katika *KcFL* ukarabati umefanywa kukawa na simulizi la moja kwa moja kama ilivyo katika dondoo lifuatalo.

*Liyongo kitakamali,*
*Akabalighu rijali,*
*Akawa mtu wa kweli*
*Na haiba kaongeya.*
*(UwFL ubeti 6)*

*Liyongo kakua mwilini, hashindiki michezoni; vigumu kuanguka chini, huwashinda wapinzani...*
*(KiKcFL uk. 2)*

Mabadiliko haya ni mfano wa wazi wa uundaji upya wa maana unaolenga kumfanya mtoto aelewe simulizi kwa urahisi zaidi. Hali kadhalika, katika *MwSHL*, beti za kishairi zinazohesabu siku za safari zimekarabatiwa kuwa taarifa fupi na wazi:

*Na mtu kitoka kitoka shaka,*
*Hata pate ukafika,*
*Siku nne kwa haraka...*
*(UwFL ubeti 5)*

*... ilimchukua Liyongo siku mbili tu kutoka Shanga hadi Pate.*
*(MwSHL uk. 30)*

Hii ni mifano dhahiri ya urahisishaji wa kisarufi unaoendana na muktadha wa watoto, ambapo miundo tata ya kishairi imekarabatiwa kuwa taarifa sahili. Kwa mujibu wa Tylor (1994), lugha inapotumiwa kwa urahisi huchochea uelewa na hujenga uwezo wa kiakili wa watoto.

***Uondoaji wa Lugha ya Kishairi na Uboreshaji wa Lugha ya Mazungumzo***

Kwa mujibu wa nadharia ya Usimilisho ya Hutcheon (mtaje), usimilisho ni kitendo cha kuhamisha kazi kutoka muktadha mmoja kwenda mwingine kwa lengo la kuunda mfumo mpya wa uwasilishaji wa maana unaoendana na hadhira lengwa. Katika muktadha wa utafiti huu, ukarabati wa lugha kutoka katika mfumo wa kishairi kuelekea lugha ya mazungumzo si mchakato wa kubadilisha maneno pekee, bali ni hatua ya kimakusudi ya kifasihi inayowakilisha uumbaji upya wa maandiko ya kale ili yaweze kueleweka na kuvutia wasomaji wachanga.

Tenzi za kale kama *UwFL* na *UwMK* zilitumia lugha ya kisanaa iliyojaa taswira, sitiari, methali, na vina tata. Mbinu hizi, ingawa ni muhimu katika ujenzi wa maana, aghalabu ni ngumu kwa watoto kuelewa. Katika usimilisho wake, waandishi wa *KcFL*, *MwSHL*, na *WwMK* wamekarabati lugha hiyo kwa kuiondoa katika mfumo wa kishairi na kuiweka katika mtindo wa mazungumzo wenye uelekeo wa simulizi. Lugha imefanywa kuwa nyepesi, sahili na ya moja kwa moja ili iwiane na ulimwengu wa watoto.

*Kwa baba enda sikhini,*
*Umuulize yakini,*
*Kimuuwacho ni nini,*
*Nakuomba hili moya.*
(*UwFL* ubeti 126)

*Kwa upande wako nitahitaji tu umpeleleze babako hadi ugundue ni kitu gani kinachoweza kumuua.*
(*MwSL* uk 73)

Vielelezo vinavyoonyesha mabadiliko hayo (mfano wa beti za *UwFL* zikilinganishwa na aya katika *KcFL* na MwSHL) vinaonyesha jinsi lugha tata ya kishairi ilivyovunjwa na kujengwa upya katika muundo wa nathari.

*Na ayapo muhitaji,*
*Mama kwako simuhiji,*
*Kwa uwezalo mbuji,*
*Angusa kumtendea.*
(*UwFL* ubeti 64)

*... la muhimu zaidi kwangu ni nyinyi muwe watu wenye kuwahurumia na kuwaonea imani wenye mahitaji na wanaoteseka kwa hili au lile. Msiwe wachoyo bali wafikirieni kwanza waliowazunguka.*
(*WwMK* uk 31)

Mtindo huu mpya unaelekea katika lugha ya mazungumzo, unaoambatana na maelezo, na hisia, zinazowafanya watoto kushiriki zaidi katika hadithi. Ukarabati hu unaonyesha hoja kuu ya Hutcheon (mtaje) kwamba kila usimilisho ni mchakato wa ubunifu unaohusisha kubadili si tu maana bali pia umbo la kazi ya awali ili kuendana na mahitaji ya hadhira mpya. Kwa hivyo, urahisishaji wa lugha ya kishairi kuwa lugha ya mazungumzo ni hatua ya makusudi ya kuondoa vikwazo vya kiufahamu kwa watoto na kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika kazi za fasihi. Hivyo, urahisishaji wa lugha ya kishairi na ujenzi wa mtindo wa mazungumzo ni ushahidi tosha wa jinsi usimilisho unavyofanya kazi kama mchakato wa kubadilisha, kubuni upya na kufasiri fasihi kwa mujibu wa hadhira ya watoto.

### *Matumizi ya Lugha ya Kiutoto*

Matumizi ya lugha ya kiutoto ni mojawapo ya mbinu kuu za kuikarabatikazi ya kifasihi kutoka katika muktadha wake wa awali (tenzi za kale) na kuifanya iendane na hadhira mpya (watoto). Hutcheon anasisitiza kwamba kila usimilisho ni mchakato wa uumbaji upya unaolenga kuhamisha maana, hisia na uzoefu wa maandishi ya awali kwa njia ambayo itapokelewa na kueleweka katika muktadha mpya. Kwa mujibu wa maelezo ya Wamitila (mtaje), tenzi za kale zilitumia lugha ya kifasihi yenye uzito, sitiari, tamathali tata na msamiati wa kishairi. Lugha hiyo, ingawa ina thamani ya kifasihi, mara nyingi ni vigumu kwa watoto kuifasiri. Hivyo, katika usimilisho, waandishi wameingiza lugha ya kiutoto ambayo ina ucheshi, urudiaji wa maneno na sauti, pamoja na hali ya kimchezo inayowafanya watoto wajihusishe moja kwa moja na matini. Kwa mfano, lugha ya kishairi iliyokuwa na vina na mizani hubadilishwa katika usimilisho kuwa kauli sahili, za moja kwa moja, na mara nyingine zenye uradidi au mizaha inayofanana na michezo ya watoto. Hili linathibitisha hoja ya Hutcheon kwamba lugha ni kipengele kinachoweza kubadilishwa kwa makusudi katika usimilisho ili kuendana na saikolojia ya hadhira mpya. Hivyo basi, matumizi ya lugha ya kiutoto katika usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto ni mfano wa wazi wa mabadiliko ya kimakusudi ambayo yanathibitisha hoja ya Nadharia ya Usimilisho.

Kwa mujibu wa Alembi (1991), watoto huwa wasikivu wa sauti na huwa na uwezo wa kutambua sauti tofauti hata bila kuona asili ya sauti yenyewe. Waandishi wametumia tanakali za sauti katika masimilisho husika jambo ambalo halijajitokeza katika matini chanzi. Waandishi walitumia tanakali tanakali kama vile, *njorinjori sikizeni (KcFL* uk. 2), *ho ho* (*WwMK*, uk. 24). *falsafa kem kem* (*WwMK,* uk. 32), *eeeh...* (*WwMK* uk. 41), *hoyee..* (*WcMK* uk. 43), *vuu vuu (MwSL,* uk 1*), kunyamaza jii, ( MwSL, uk.11), bubujubububuju ( MwSL,* uk 15*), kuvifunga ki ki ki (MwSL,* uk 27*)* ili kuwashirikisha watoto kihisia. Tanakali hizi, ambazo hazipo katika tenzi chanzi, hujenga taswira za sauti na kuongeza usikivu wa watoto.

Kulingana na Wamitila (2000) na Wafula (1994), methali ni kauli zilizokubalika katika utamaduni wa jamii. Methali zimekarabatiwa kutoka lugha ngumu ya kale hadi kauli rahisi zinazofundisha maadili. Katika *WwMK*, methali kama *mapenzi ni kikohozi hayawezi kufichika* (*WwMK*, uk. 23) na *akipenda chongo huita kengeza* (*WwMK*, uk.26), zinatumiwa kuelimisha watoto kuhusu mapenzi na upendo wa kweli. Vilevile, *MwSL* hulitumia methali kama *chochote king'aacho si dhahabu* (*MwSHL*, uk. 26). na *mbio za sakafuni huishia ukingoni* (*MwSHL*, uk. 50) kuwaonya watoto dhidi ya tamaa na matendo ya pupa.

Kwa mujibu wa Alembi (1991), watoto hufurahia nyimbo katika matini kwa sababu wanaweza kuimba na pia kuambatanisha wimbo na miondoko na matendo kama vile kupiga makofi. Nyimbo na ngoma zimeingizwa katika masimilisho teule ili kuongeza mvuto, furaha na mawasiliano kwa watoto. *WwMK* ina nyimbo za harusi kama:

"*Hongera mwanangu hongera, mama uchungu, hoyee*…" *WwMK k 43)*

Nyimbo hizi huchochea ushiriki wa watoto, hufundisha kuhusu desturi za jadi na zinawaunganisha na utamaduni wa Kiafrika. Katika MwSL, ngoma ya gungu na mwao inatumika si tu kwa burudani, bali pia kama chombo cha kuwasilisha ujumbe wa kificho kwa mfano, Liyongo kutumia wimbo kufikisha ujumbe kwa mama yake ili apate uhuru *(MWSL* uk 56). Hivyo, nyimbo na ngoma ni nyenzo za mawasiliano, burudani na elimu.

Kulingana na Wamitila (2003), chuku huliweka jambo ambalo linazungumziwa katika kazi ya fasihi kwa uwazi zaidi, huku ikikuza sifa fulani. Chuku ilitumika katika masimilisho teule kuongeza fantasia na mvuto wa hadithi. Kwa mfano, katika *KcFL*, Liyongo alielezwa kuwa alikunywa debe la maziwa

mara tu alipozaliwa hali inayokuzwa zaidi ili kumvutia mtoto. Hii inaibua taswira za kishujaa na kuimarisha kipengee cha fantasia kinachopendwa na watoto. Vivyo hivyo, katika *WwMK*, Zuhura anaelezewa kuwa aliposwa kwa mwaka mzima bila kumwona mchumba wake, jambo lililotiwa chuku ili kubainisha desturi za kale kwa njia ya kuvutia.

Watunzi wametumia semi kama methali, mafumbo na nahau kuendeleza maudhui kwa namna nyepesi na ya kimafunzo. Mafumbo yalitumika kama njia ya kuhimiza kufikiri kwa watoto huku yakibeba maana fiche inayowashirikisha watoto katika tafakari. Lugha ya semi huwafanya watoto kuwa wabunifu, wadadisi na waelewa zaidi wa maadili ya kijamii. Katika *WwMK*, mwandishi alionyesha jinsi ami wa Said alitumia fumbo la "mbegu" kumrejelea Zuhura, akionyesha ubunifu unaofaa kwa hadhira ya watoto. Aidha, fumbo la "kasha la zamani" katika sura ya tatu linatumika kuonyesha thamani na uadilifu wa mke, ambapo mume anamfananisha mkewe na kasha alilolifunga na kutunza kwa wivu. Vilevile, matumizi ya taswira katika *MwSL*, *KcFL* na *WwMK* yalijenga picha halisi akilini mwa mtoto. Kwa mfano, taswira ya urembo wa Shida katika *MwSL* (uk.25), ya Moni akimsukumia msumari babake (uk.86), ya Liyongo akipambana na mamba katika *KcFL* (uk.3) na mashua ikisukumwa na upepo katika *WwMK* (uk.76) zote zinamwezesha mtoto kuunda picha ya matukio na wahusika. Hivyo, matumizi ya semi na taswira yanathibitisha kwamba lugha katika usimilisho wa tenzi za kale iliboreshwa kuwa ya kuvutia, ya kufundisha na rahisi kueleweka kwa watoto, ikizingatia saikolojia na uwezo wao wa kufikiri.

Waandishi wa masimilisho teule walitumia picha zilizotiwa rangi kama nyenzo muhimu ya usanii na mawasiliano katika kuwasilisha tenzi za kale kwa watoto. Kwa mujibu wa Tucker (1984), watoto huvutiwa na vitabu vyenye picha zenye rangi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Usimilisho, Andrew (1985) anasema kuwa, matumizi ya picha zenye rangi ni sehemu ya mchakato wa kubadilisha na kuunda upya maana ili iendane na hadhira mpya. Katika *KcFL*, picha kama za kuzaliwa kwa Liyongo (uk.2), pambano na mamba (uk.3) na vita dhidi ya Sango Bili (uk.5) zinajenga taswira ya ujasiri na ushujaa huku zikisaidia watoto kuelewa imani na hadithi za kishujaa za jadi. Vivyo hivyo, *WwMK*, picha za wanawake sokoni (uk.23), Mwana Kupona akiandika utenzi (uk.49) na mandhari ya bahari na mashua (uk.68, 76) zinawaingiza watoto katika ulimwengu wa maisha ya Pwani. Kadhalika, katika *MwSL*, picha za Liyongo akipuliza panda (uk.29), kushiriki mashindano (uk.13) na akiwa mbaroni (uk.46) zinajenga hisia za kishujaa na huruma. Kwa watoto, picha hizi si pambo bali ni zana za kiakili na kihisia zinazorahisisha uelewa na kuongeza ushiriki katika simulizi. Kwa kuzingatia mtazamo wa Hutcheon (2013), matumizi ya picha yanadhihirisha kuwa usimilisho si mabadiliko ya kimaumbo pekee bali ni mbinu ya kufanikisha mawasiliano kulingana na saikolojia ya watoto.

### *Kupunguza Uzito wa Dini na Lugha ya Kiunabii*

Kwa mujibu wa TUKI (2013), dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho na mfumo wa kuabudu na kumtii Muumba. Muhammad (2010) anafafanua Uislamu kama hali ya kujisalimisha kwa Mungu kwa kumpwekesha na kumtii. Katika usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto, kumekuwa naukarabati wa kimaudhui na kimaumbo hasa katika kupunguza uzito wa dini na lugha ya kiunabii ili kuelekea lugha nyepesi na simulizi za kijamii. Kwa mujibu wa Nadharia ya Usimilisho, Starrs (2006) anasema kuwa ukarabati wa maudhui si upotevu wa maana bali ni mbinu ya kusahilisha uwasilishaji wa ujumbe ili uendane na hadhira mpya, yaani watoto, ambao wana uwezo mdogo wa kufasiri lugha nzito za kiimani. Katika UwMK, Mwana Kupona anamnasihi binti yake kwa kutumia lugha ya dini na mafundisho ya Kiislamu (beti 12, 22 na 23), akisisitiza utekelezaji wa nguzo za dini. Katika usimilisho wa UwMK; WwMK, mafundisho hayo yamewasilishwa kwa lugha rahisi na mifano ya kijamii bila

kuhusisha mafundisho ya moja kwa moja ya dini jambo linalorahisisha uelewa wa watoto. Vivyo hivyo, UwFL unaanza kwa dua na kumtukuza Mtume Muhammad (S.A.W), lakini katika masimulizi yake ya watoto, MwSL na KcFL, marejeo hayo yameondolewa na badala yake Liyongo amewasilishwa kama shujaa wa kijamii anayepambana na dhuluma kwa hekima na ujasiri. Mabadiliko haya yanaonyesha kwamba usimilisho umeepuka lugha ya kiunabii na badala yake umejikita katika maadili, ujasiri na utu ili kuendana na mazingira ya ukuaji wa watoto.

### *Kipengele vya Maudhui*

Kwa mujibu wa nadharia ya Usimilisho ya Hutcheon (mtaje), kuhamisha tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto ni mchakato wa kubadilisha maana na maudhui ili yaendane na uelewa, matarajio na mahitaji ya hadhira mpya ya watoto. Mabadiliko haya yanaonekana wazi katika mada kuu kama ujasiri, udhaifu, ushirikiano, ufadhili, upendo na urafiki. Katika *UwFL* na *UwMK*, mada hizi ziliwasilishwa kwa mtazamo wa kishujaa, kifalsafa na kidini zikilenga watu wazima, ilhali katika *MwSHL*, *KcFL* na *WwMK*, mada hizo zimetafsiriwa upya ili ziwe rahisi kueleweka na kuvutia watoto. Ujasiri wa kivita katika *UwFL* umegeuzwa kuwa ujasiri wa kijamii na kimaadili unaomfundisha mtoto kuwa jasiri katika hali za kawaida za maisha huku udhaifu ukionyeshwa kwa lugha ya huruma badala ya mateso makali. Vivyo hivyo, mada za ushirikiano, upendo na urafiki zimepewa sura ya maisha ya kila siku ya mtoto kama kusaidiana nyumbani, kushirikiana michezoni na kujali wanyonge kama inavyoonekana kupitia wahusika wa *WwMK*, *KcFL* na *MwSL*. Fadhili ambazo katika tenzi asilia ziliambatana na wajibu wa kijamii na kidini, katika masimilisho ziliwasilishwa kama maadili ya utu na ushirikiano wa kijamii kupitia mifano ya matendo mema kwa wanyama na wanadamu. Hivyo, kwa mujibu wa Hutcheon (mtaje), usimilisho haujengi nakala dhaifu ya kazi ya awali, bali ni uumbaji upya unaodumisha kiini cha maadili na urithi wa kitamaduni huku ukizielekeza kwa namna inayokubalika katika ulimwengu wa mtoto.

### *Kipengee cha Wahusika*

Kulingana na Mbatiah (2001), wahusika ni viumbe ambao hupatikana katika kazi ya fasihi. Wahusika hudokeza kuhusu ujumbe wa kazi ya fasihi kutokana na matendo na mazungumzo yao. Wahusika katika tenzi za kale aghalabu huwa watu wazima, mashujaa au viumbe wa hadithi. Wahusika katika tenzi za kale kama *UwFL* na *UwMK* walikuwa watu wazima, mashujaa na viongozi wa kidini, lakini katika masimilisho kama *MwSHL*, *KcFL* na *WwMK*, wahusika hao wamekarabatiwa, wahusika wapya wakabiniwa upya na kuongezwa ili watoto waweze kujinasibisha nao na kujifunza maadili. Fumo Liyongo, kwa mfano, amesawiriwa katika matini chanzi kama shujaa jasiri na mwenye hekima, ilhali katika masimilisho amebadilishwa kuwa kijana mwenye ujasiri na udhaifu, hivyo kumpa mtoto nafasi ya kujifunza kuwa hata mashujaa hukosea na hubadilika. Saada ameongezewa sifa za utiifu na uaminifu, Mbwasho amepewa nafasi kubwa zaidi kama mama mwenye hekima na ujasiri na Halali ameongezwa kama mhusika mpya anayeonyesha hasara za wivu na tamaa. Vivyo hivyo, katika *WwMK*, wahusika wapya kama Zuhura na Fatuma wametumika kuonyesha maadili ya urafiki, utiifu na mshikamano huku wanyama kama ngamia na paa wakitumika kama wahusika wanaowakilisha matendo ya kibinadamu ili kuwavutia watoto. ukarabati huu unaendana na hoja ya Hutcheon (mtaje) kwamba, usimilisho si kunakili bali ni kubuni upya ili kuunda maana mpya. Hivyo, kupitia kubadilisha tabia, majina na uhusiano wa wahusika, waandishi wameunda mazingira yanayomjenga mtoto kimaadili, kihisia na kijamii huku wakihifadhi kiini cha kihistoria na kitamaduni cha kazi asilia.

### 1.7 Hitimisho

Kuna ushahidi wa ukarabati wa vipengee vya tenzi za kale kutoka usimulizi wa kifasihi cha kishairi kilichokuwa na lugha ngumu na taswira nzito za kidini na kihistoria, kuelekea fasihi ya watoto iliyo rahisi kusomeka, yenye msamiati mwepesi na simulizi zinazohusiana moja kwa moja na maisha ya kila siku ya watoto. Kwa jumla, usimilisho wa tenzi za kale umeonyesha ukarabati wa lugha, maudhui, wahusika na muundo. Ingawa ladha ya kishairi na uzito wa kifasihi wa jadi umepunguzwa, usimilisho umefanikisha lengo kuu la kuhakikisha kwamba historia, tamaduni na mafunzo ya kale yanaendelezwa kwa vizazi vipya. Usimilisho wa *UwMK* na *UwFL* unatoa fursa ya kuunda hadithi mpya ambazo zinakuza maadili, zinawasisimua watoto na zinachangia katika kukuza utamaduni wa Kiswahili. Hivyo, ni muhimu kwa waandishi wa fasihi ya watoto kufahamu na kuyatumia vizuri maarifa haya ya kale ili kuunda kazi zinazoweza kuhamasisha na kufundisha watoto kwa njia bora zaidi.

### Marejeleo


Alembi, E. "Analysis of the Style and Social Significance of the Abanyole Children's Poetry". Tasnifu ya uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Andrew, D. (1984). *Concepts in Film Theory*. New York: Oxford University Press.

Baker, M. (2001). *Routledge Encyclopedia of Transilation Studies*. London: USA Routledge.

Balodis, J.M (2012) "The Practise of Adaptation: Turning Fact and Fiction Into theatre." Doctoral dissertation. Ph. D Thesis, Queensland University of Technology. https://eprints.qut.edu.au/60917/1/Janis_Balodis_Thesis.pdf. Accessed on 3/2/2023.

Bluestone, G. (1957). *Novels into Film*. Berkeley: University Press.

Dean, J. (2009). "Adaptating History and Literature into Movies", In *American Studies Journal*. Vol 1. No. 53

Goodman, N. (1976). *Languages of Art*. Indianopolis: Hacket.

Hutcheon, L. (2013). *A Theory of Adaptation*. New York: Routledge.

Kairu, W. M. (2005). "Uhalisia na Mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya Watoto." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Kaui, M. (2015). Tathmini ya Usimilisho wa riwaya na Hadithi Fupi kwa Wanafunzi wa Sekondari Nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

King'ei, K. (2008). *Wasifu wa Mwana Kupona*. Nairobi: Sasa Sema Publishers Limited.

Lhermitte, C. (2005). "A Jakobsonian Approach to Film Adaptation of Hugos Les Miserables" In *NEBULA: A Journal of Multidisciplinay Scholarship* pp. 97-107. *http://www.nobleworld.biz/nebulaarchive/nebula21.html.* Accessed 22/1/2023.

Matundura, B. (2018). *Mkasa wa Shujaa Liyongo*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mohamed, S.A. (2010). Kunga za Nathari ya Kiswahili Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mwendwa, S. (2020). "Usimilisho wa Vielelezo katika Hadithi za Watoto na Namna Vinavyochangia katika Uwasilishaji Ujumbe." Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapoishwa)

Ngugi, P.M. Nabea, W. (2011). Children's Literature in Kiswahili: A Stylistic Approach katika *East African Literature: Essays on Written and Oral traditions*. Logos: Verlag Berlin. Kur. 223-244

Ngugi, P. (2011). *Language and Literacy Education: The State of Children's in Kiswahili in Kenya.* London: Lambert Academic Publishing Press.

Njogu, K. na R. Chimerah, (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F. (1979). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Omuya, R. (2017). "Usimilishwaji wa Biblia kama Fasihi ya Watoto." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Punzi, M. P. (Mhr) (2007). *Literature Intermediality: The Transit of Literature Through the Media Circuit*. Germay: International academic Publishers.

Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*. India: Meveli Publishers.

Sanders, J. (2006). *Adaptation and Appropriation. The New Critical Idioms*. London: Routledge.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi Andishi*. Dar es Salaam: Kauttu Limited Press.

Starrs, D. B. (2006). "A Queer New World: Adaptation Theory and the Zeugma of Fidelity in Derek Jarman's The Tempest." The University of Melbourne, Vol 1. *http://docs.google.com*. Accessed *16/8/2023*

Tucker, N. (1984). *The Child and the Book*. Cambridge: Printed in Great Britain at the University Press.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Wafula, R.M. (1994) "Uainisho wa Methali". *Writers Forum Journal of the Writes' Association of Kenya,* Juz 2A: 63-68.

Wamitila, K. W. (2000). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide - Muwa Publisherss.

_______________ (2002). *Uhakiki wa Vitabu: Misingi na vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers

_______________(2003) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books Limited.

_______________ (2007). *Kisa cha Fumo Liyongo- Hadithi za Mashairi 8*. Nairobi: Vide - Muwa Publisherss.

**Viambatisho**

***Kiambatisho 1: Utenzi wa Mwana Kupona (Mulokozi, 1999)***

1. La tatu uwe sadiqi,
Ushikalo ulithiqi,
Mtu asoshika haqi,
Sandamane naye ndiya.
2. Ifanye mteshiteshi,
Kwa maneno yaso ghashi,
Wala sifanye ubishi,
Watu wakayatukiya.
3. Naawe radha mumeo,
Siku zote mukaao,
Siku mukhitariwao,
Awe radhi mekuwiya.
4. Na ufapo wewe mbee,
Radhi yake izengee,
Wende uitukuzie,
Ndipo upatapo ndiya.

40. Nyumba yako inadhifu,
Mumeo umsharifu,
Wakutanapo sufufu,
Msifu ukimtaya.

41. Muyuwe alipendalo,
Nawe lifuate lilo,
Yambo limtukialo,
Siwe mwenye kumweteya.
64. Tamati maneno yangu,
Kukuusia mwanangu,
Sasa tumuombe mungu,
Anipokelee dua.

***Kiambatisho 2: Utenzi wa Fumo Liyongo (Mulokozi, 1999)***

6. Liyongo kitakamali
Akabalighu rijali
Akawa mtu wa kweli
Na haiba kaongeya
7. Kimo kawa mtukufu
Mpana sina mrefu
Majimboni yu marufu
Watu huya kwangaliya.
10. Sulutwani pate bwana
Papo naye akanena
Wagala mumemuona
Liyongo kiwatokeya?"
12. Mfalme kawambiya
Wagala kiwasifiya
"huwegema watu miya
Wasiweze hukimbiya.
13. "Ni mwanamume swahihi
Kama samba una zihi
Usiku na asubuhi
Kutembea ni mamoya
14. Ghafula kikutokeya
Mkoyo hukupoteya
Tapo likakuwiliya
Ukatapa na kuliya
15. Mato kikukodoleya
Ghafula utazimiya
Kufa kutakurubiya
Kwa khaufu kukungiya
16. Wagala wakipulika
Kwa dhihaka wakateka
Wakanena"twamtaka
Na sisi kumwangaliya"
21. Na liyongo akajibu
Kwa hishima na adabu
" nitakuja kwa karibu
Nitwiiye maulaya"

25. Na mtu kitoka shaka
Hata pate ukafika
Siku nne kwa haraka
Alo hodari sikiya

26. Liyongo akikabili
Ndiya kenenda rijali
Alikwenda siku mbili
Na ya pili ni kungiya

28. Kiivuzia hakika
Muini wakashituka
Panda ikapasuka
Wagala wakasikiya

37. Kisa katiti katuwa
Mkobani akatowa
Zitu alizotukuwa
Nyumba ndima nisikiya.

101. Na mamake kwa hakika
Chakula chema kipika
Asikari humpoka
Chakula wakailiya

126. "kwa baba enda sikhini
umuulize yakini
Kimuuwacho ni n"ni
Nakuomba hili moya

228. Tumeziya kukhitimu
Hapo ndio wasalamu
Ilahi tatukirimu
Kwa Baraka na afiya

229. Rabi tatusahiliya
Na uzito wa duniya
Tena tatujaaliya
Kuwa njema yetu niya